



Utangulizi

Ni nini maana ya kuhesabiwa haki?

Ni kuachiwa huru mahakamani – kukutwa kwamba huna hatia. Popote pale neno hili ‘kuhesabiwa haki’ linapotumika katika Agano Jipya, neno ‘kuachiwa huru mahakamani’, linaweza kutumika badala yake. Neno hili linatumika katika Agano la Kale kuhusiana na haki za binadamu. Mfano Isaya 5:23 na Methali 17:15, ingawa hapa pia tunakuta kwamba katika tafsiri za kisasa mara kwa mara zinatumiya neno, ‘kuwekwa huru’.

Kuhesabiwa haki ni ile hali ya muumini wa kweli kupitia neema ya Mungu anajikuta kuwa hana hatia. Ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu wanayopewa wale wote wamuaminio Yesu – Ni hakimu mwenyewe ambaye anawatangazia waumini ya kwamba hawana hatia. Katika Ukristo muumini wa kweli anakutwa hana hatia kwamaana adhabu ya dhambi zake imekwisha kubebwa na Yesu.

Kuhesabiwa haki maana yake ni zaidi ya msamaha

Ni msembo ambao ni wa mahakama ya sheria. Mshtakiwa anaweza kuhukumiwa adhabu ama kuhesabiwa haki – maoni juu ya matendo yake yanaelekeza kwamba hana hatia ama ana hatia kwa kuvunja sheria. Mtu asiye na hatia ni mtu aliye na haki, na hakimu ambaye anathibitisha kuwa mtu huyu ana haki ndiye anayemhesabia mtu huyu haki. Neno lingine la kisasa ambalo lina maana hii hii ni neno, uthibitisho. Kuhesabiwa haki hakumfanyi mtu mwenye dhambi kuwa tofauti: kunamfanya mtu huyu kuwa na haki mbele ya sheria. Ni hakika kwamba mtu mwenye dhambi anapaswa kufanywa kuwa mtu mwema, na Roho Mtakatifu ataendelea kusaidia kumfanikisha kufikia lengo hilo katika maisha ya waumini, katika kile kijulikanacho kama ‘utakaso’. Kuhesabiwa haki hakuhusiani na hali yetu tuliyonayo bali na msimamo wetu – inahusu nafasi tulionayo mbele za Mungu. Mbali na Kristo hatuna nafasi yoyote; tunahatia na tunastahili hukumu. Kristo ni Mwokozi wetu na pia anasimama badala yetu ambapo sisi tunahesabiwa haki na kuachiwa huru – Yesu amezichukua dhambi zetu yeye mwenyewe.

Isaiah **50:8**; Yohana **5:24**; Warumi **3:19, 20, 25, 26**; **4:5, 8**; **8:31-34**; 1 Wakorintho **1:30**;
2 Wakorintho **5:21**

Waumini wanahesabiwa haki kwasababu Yesu alizibeba dhambi zao pale msalabani.

Mungu, kama hakimu, ametangaza kwamba wale wanaomuamini Kristo kwamba ni Mwokozi wamehesabiwa haki na wana haki pia.

Warumi **4:25**; **5:9**; **8:1**

Kuhesabiwa haki ni kwa neema peke yake

Ni pasipo kustahili, na kwa maneno ya mtume Paulo, si kwa matendo ya haki ambayo tumeyafanya. Matendo mema, jitihada katika kusihi, kujitoa sadaka, na hata kutoa mali zote hakuna thamani ya milele.

Yohana 3:17-18; Warumi 3:24, 28-30; 5:16-18; Wagalatia 2:16; 3:8, 11, 24; 5:4; Luka 18:14

Tunapaswa kukubali hatia tuliyonayo mbele za hakimu mwenye haki

Ni hapo tu ndipo tunaweza kuhesabiwa haki kwa imani. Baada ya hapo maisha yetu yanapaswa kuwa ni ya ushuhuda juu ya imani yetu.

Waefeso 2:8-10; Tito 3:4, 5, 7; Yakobo 2:21-24; 1 Yohana 1:9

Hitimisho

Kuhesabiwa haki na kuwa mwenye haki kuna maana ile ile katika maeneo mengi ya maandiko matakatifu. Warumi 5:1-11 ni ufupisho mzuri wa matokeo ya kufurahisha ya kuhesabiwa haki (au kuwekwa huru) mbele za Mungu.

Dhana ya 'kuhesabiwa haki' inapaswa kutazamwa pamoja na maana ya kuwa 'mwenye haki'. Tunapaswa kuzingatia hasa ukamilifu na haki takatifu ya Mungu.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK
www.sovereignworldtrust.org.uk

Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.
Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - www.christian-publications-int.com
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4